

## **Kupunguzwa kwa malipo ya chekechea (barnehage) / utunzaji wa mchana shuleni -SFO kuanzia juni 2021**

### **CHEKECHEA**

#### **Kupunguzwa kwa malipo ya wazazi kwa familia au nyumba ambazo zinapokea mshahara chini ya krona 592.167 kwa mwaka**

Wale ambao wanaishi katika nyumba moja na mapato au mshahara wao kwa jumla/mwaka ni chini ya krona 592.167 kwa wanaweza kuomba ili wawapunguziwe malipo ya chekechea. Kumbuka kwamba ikiwa una watoto kadhaa, ni lazima utume ombi kwa kila mmoja wa watoto hawa.

#### **Wakati wa msingi bila malipo kwa nyumba ambazo zina mshahara au mapato chini ya krona 583.650 kwa mwaka**

Wakati wa msingi bila malipo inamaanisha kwamba mtoto mmoja hushiriki masaa 20 ya katika chekechea kwa wiki bila malipo. Unaweza kupata nafasi ya wakati wa msingi bila malipo kutoka mwezi wa nane mwaka ule mtoto wako anafikisha umri wa miaka 2. Ikiwa utaomba malipo ya mzazi yaliyopunguzwa, utapokea moja kwa moja nafasi ya wakati wa msingi bila malipo ikiwa mshahara wa familia uko ko chini ya krona 583.650 kwa mwaka.

### **Utunzaji wa mchana - SFO**

#### **Kupungunziwa kwa malipo ya wazazi kwa nyumba zenya mshahara/mapato chini ya krona 505 083 kwa mwaka**

Wale ambao wanaishi katika nyumba au familia moja na mapato yao kwa mwaka ni chini ya NOK 505 083 wanaweza kuomba kupunguziwa malipo ya wazazi katika SFO.

#### **SFO bila malipo kwa watoto wa darasa la 1 kwa nyumba ambazo zina mapato au mshahara chini ya krona 350.000 kwa mwaka**

Ikiwa unaomba kupunguziwa malipo ya mzazi katika SFO, utapata SFO bila malipo mara moja kama mtoto wako yupo katika darasa la kwanza na nyumba yako ina mapato ambayo iko chini ya krona 350.000 kwa mwaka.

### **Jinsi ya kuomba**

Unaomba kielektroniki. Ambatanisha na nyaraka au karatasi halali. Unaingia kwa kutumia kitambulisho rasmi - ID porten (Kitambulisho cha Benki-Bank ID, Kitambulisho cha kibinafsi-MIN ID n.k.) ili kutuma maombi yako.

### **Fomu ya maombi inaweza kupatikana hapa:**

[www.bergen.kommune.no/redusert-foreldrebetaling](http://www.bergen.kommune.no/redusert-foreldrebetaling)

## **Ni nyaraka zipi ambazo ni halali**

- Muhtasari wa malipo ya kodi (repoti ya malipo) - skattemelding - ya mwaka wa 2020 ya watu wazima katika nyumba ambayo mtoto anaishi pamoja nao ni lazima iambatanishwe na barua ya maombi
- Ikiwa kuna mabadiliko makubwa katika mapato yako kulingana na ripoti ya malipo, unaweza pia kuambatanisha hati za mshahara kwa miezi 3 iliyopita. Ikiwa umefutwa au umepoteza kazi, unaweza kuambatanisha nyaraka kutoka kwa aliyekuwa mwajiri wako
- Uamuzi kuhusu msaada kutoka hazina ya mkopo wa kielimu -studie lånekassen na cheti cha uanafunzi
- Uamuzi kutoka kwa NAV ya kijamii - sosial / kumalizika kwa kipindi cha uamuzi kutoka kwa NAV ya kijamii
- Ikiwa unasubiri ufafanuzi-avklaring kutoka kwa NAV, ni lazima uthibitishwe hii kwa maandishi rasmi
- Habari zingine muhimu kuhusu mapato yako ya sasa

### **Ikiwa hauna muhtasari/repoti ya malipo ya kodi - skattemelding**

Kila mtu ambaye amekuwa akiishi Norway kwa mwaka uliopita ana hati ya kodi au ripoti ya malipo /ushuru ni lazima aiambatanishane na maombi hayo. Ikiwa umefika tu Norway na hauna malipo ya ushuru, lazima uambatanishe na nyaraka za kibali cha kuishi nchini Norway.

### **Maombi haya yanahusu kipindi gani**

Maombi ya kupunguziwa kwa malipo ya wazazi yanahusu kutoka mwezi unaofuata baada ya maombi kupokelewa. Utatumiwa uamuzi( jibu) baada ya ombi lako kukubaliwa.

### **Ikiwa hauna nambari ya kijamii ya kujitambulisha-personnummer / hauwezi kuomba kielektronik**

Unaweza kuwasiliana au kuongea na manispaa ya Bergen, Huduma ya huduma ya Raia-innbyggjerservice katika Kaigaten 4. Hapo utapewa msaada wa kutuma maombi kielektroniki au kwa njia ya kawadia ikiwa hauna nambari ya kijamii ya kujitambulisha. Lete kitambulisho halali na nyaraka zinazohitajika kwenye maombi. Ofisi ya huduma ya raia inatumia nambari hii ya simu 55 56 55 56.

### **Muhimu! Kumbuka kutumba ombi kila mwaka wa mtoto kushiriki chekechea**

Maamuzi juu ya kupunguziwa kwa malipo ya wazazi inahusu maramoja kila mwaka. Ni lazima utume ombi jipya kabla ya mwezi wa nane ili upate malipo ya yaliyopunguzwa katika mwezi wa nane.